# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI

ISSN2507-8797X Toleo No 5 2023/2024




## KARIBU MWENGE WA UHURU KINONDONI

## MEI 11, 2024

"TUNZA MAZINGIRA NA SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA KWA UJENZI WA TAIFA ENDELEVU"



# KARIBU MWENGE WA UHURU KINONDONI




**MHARIRI MKUU**
*Aquilinus Shiduki*

**MHARIRI MSAIDIZI**
*Beatha Singano*

**WAPIGA PICHA**
*Kaunga Maulid*
*Filbert Odilo*

**MSANIFU JARIDA**
*Jamila Mdemu*

**WAANDISHI**
*Athuman Ntafumila*
*Diana Kamasho*
*Sauma Mwanshuli*
*Diana Mmari*
*Kaunga Maulid*

*JARIDA HILI LIMETOLEWA NA*
*KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI*
*HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI*
*S. L. P, KINONDONI, 31902 DSM*
*SIMU: +255222170173*
*BARUA PEPE: md@kinondonimc.go.tz*


Ikiwa ni siku chache baada ya Mwenge wa Uhuru kuzinduliwa katika Mkoa wa Arusha na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inaukaribisha Mwenge wa Uhuru 2024 katika Wilaya ya Kinondoni. Mwenge wa Uhuru 2024 wenye kauli mbiu isemayo ***"Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu,"*** utakimbizwa katika miradi mbalimbali ndani ya Wilaya ya Kinondoni sambamba na uzinduzi pamoja na uwekaji wa jiwe la msingi kwenye miradi mbalimbali. Katika uzinduzi huo Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa amehimiza vijana kuacha matumizi ya madawa ya kulevya ili kuongeza nguvu kazi ya taifa zima.

# TAHARIRI

## MUUNGANO WETU, TUUIMARISHE ZAIDI

Aprili 26 ya Kila mwaka, nchi yetu husherehekea Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mwaka 1964 nchi hizi mbili ziliungana na kuzaa nchi moja, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwaka huu, Muungano wetu umetimiza miaka 60 tangu kuasisiwa kwake. Katika kipindi hiki cha miaka 60 ya Muungano, Wananchi wa pande zote mbili wamenufaika na mambo mengi kupitia maeneo 22 ya Muungano. Maneo haya yapo katika Nyanja za Kisiasa, kiuchumi na Kijamii. Hii inathibitishwa na kuimarika kwa utaifa, amani na utulivu na hali ya maisha ya wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi wa pande zpote mbili za Muungano. Pia, utekelezaji wa mambo ya Muungano kwa mujibu wa Katiba na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yale yasiyo ya Muungano unakwenda sanjari na mipango, sera, programu na mikakati ya maendeleo ambayo Serikali zote mbili zilijiwekea kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa Watanzania.



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza akitoa taarifa ya miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa ndani ya Mnaispaa ya Kinondoni.*

Kwa upande wa Manispaa ya Kinondoni, Miaka 60 ya Muungano imekuwa na maana kubwa kwetu kwa kuendeleza undugu na ushirikiano na wenzetu wa Zanzibar. Moja ya mikakati ya Manispaa ya Kionondoni ni kuanzisha na kuimarisha mahusiano ndani na nje ya nchi yetu. Kwa upande wa ndani ya nchi yetu, Manispaa yetu imekuwa na ushirikiano wa karibu na Manispaa ya Mjini (Zanzibar) kwa miaka mingi sasa. Ushirikiano huu ni moja ya faida kubwa za Muungano unaofikisha miaka 60 sasa, ambao bila kuwepo kwa Muungano huu, pande hizi mbili huenda zisinge shirikiana kama zilivyo leo. Ushirikiano huu umezisaidia pande hizi Mbili kubadilishana uzoefu katika utendaji kazi, mfano katika masuala ya ukusanyaji mapato, Uchumi wa Buluu, Usafi na utunzaji wa mazingira. Pande hizi mbili zimekuwa na utaratibu wa kutembeleana na kubadilishana uzoefu mara kwa mara. Hatua hii imesaidia, siyo tu katika utendaji, bali pia katika kukuza udugu baina yetu. Tunapoanza safari nyingine ya Miaka 60 ya Muungano, ni matarajio yetu kuwa Manispaa zetu Mbili za Kinondoni na Mjini, zitaimarisha zaidi ushirikiano katika Sekta nyingine zikiwemo za Elimu na Afya. Lengo likiwa ni kuboresha zaidi maisha na uchumi wa kila mtanzania mahali alipo. Katika kusherehekea miaka 60 ya Muungano wetu, Sisi wana-Kinondoni, tunatoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, pamoja na viongozi wote waandamizi wa Serikali zote mbili kwa kuendelea kuulea Muungano wetu. Sisi, Manispaa ya Kinondoni, tutazidi kuuenzi Muungano huu kwa faida ya Manispaa yetu. na Manispaa ya Mjini.

# KINONDONI KUKABILIANA NA KIPINDUPINDU

**Na JAMILA MDEMU**

Kufuatia mfululizo wa mvua zinazoendelea kunyesha Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeweka mipango madhubuti katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko hasa ugonjwa wa Kipindupindu endapo itatokea. Hayo yalibainishwa April 12, 2024 na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mheshimiwa Saad Mtambule katika kikao chake na Watendaji wa Mitaa, Maafisa Afya na Wenyeviti wa Mitaa kilichokuwa na lengo la kuweka Mikakati hiyo. Akizungumza katuka kikao hicho Mkuu wa Wilaya alisema, "Tujiimarishe kwa kuweka mkazo katika kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu. Tusimamie na tuhamasishe wananchi kufanya usafi, kuondoa taka oza na ngumu ili kurahisisha maji ya mvua kupita kwenye njia yake vizuri bila kikwazo." Ameongeza kuwa ni wajibu wa kila mmoja kuweka nguvu katika kutokomeza maambikizi. "Viongozi kaeni na Wananchi katika kutoa elimu na hamasa dhidi ya kuacha kutiririsha maji machafu". Aidha, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza amewataka Wenyeviti wasimamie vizuri suala la usafi kwenye maeneo yao kwa kusimamia Sheria za utupaji taka ovyo."Tuonyeshane ushirikiano katika maeneo yetu kwa kuwachukulia hatua kwa wanaotupa taka ovyo na kutiririsha maji ovyo". Bi. Hanifa ameongeza kuwa, viongozi wahamasishe usafi katika maeneo yao na kutatua changamoto atika maeneo hatarishi. Kwa upande wake Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kinondoni, Dr. Ezra Ngereza, alieleza



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mheshimiwa Songoro Mnyonge (kushoto) akiambatana na wageni kutoka Ujerumani waliodhuru kiwanda cha uchakataji taka cha Mabwepande.*

kuwa Kitengo cha Afya kimeandaa Mikakati ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa huu ikiwemo kutoa elimu ya afya kwa wananchi, jamii kupata maji safi na salama. Alisema, "tumeunda timu itakayotembelea nyumba kwa nyumba ili kujua kama kuna maambukizi na kuzuia uuzaji wa vyakula kiholela." Aidha, Afisa Mazingira wa Manispaa ya Kinondoni. Bw. Shedrack Maximilian aliwasisitiza Watendaji na Wenyeviti hao kudhibiti uchafu katika maeneo yao.





# TUMIENI NISHATI SAFI ILI KUTUNZA MAZINGIRA MHE. SONGORO

**Na**
**KAUNGA MAULID**
**WW**

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mheshimiwa Songoro Mnyonge asisitiza matumizi ya nishati safi ili kuokoa uharibifu wa mazingira unaosababisha mabadiliko makubwa ya tabia nchi.

Mheshimiwa Songoro aliyasema hayo Aprili 20, 2024 katika uzinduzi wa kampeni ya usafi wa mazingira na matumizi ya nishati safi uliofanyika katika Kata ya Mikocheni Mtaa wa Michungwani, Manispaa ya Kinondoni.

Alisema, "Katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha, niwaombe wakazi wa Mikocheni na viunga vyake vyote kutunza mazingira. Hili ni jukumu letu. Tufanye usafi na kutumia nishati safi ya gesi."

Aidha Mheshimiwa Songoro amempongeza Mheshimiwa Rehema Mandingo, ambae ni Diwani wa Viti Maalumu, kwa kuanzisha kampeni hiyo ikihamasisha pia matumizi ya nishati safi. Kampeni hiyo, itasaidia Kata ya Mikocheni na Wilaya ya Kinondoni kwa ujumla kujikinga na magonjwa ya mlipuko.




Kwa upande wake Mheshimiwa Mandingo aliwashukuru Wanawake wa Kata ya Mikocheni kwa kujitokeza katika kuunga mkono kampeni hiyo yenye kauli mbiu "Wanawake na Mazingira."

Kadhalika, Mheshimiwa Mandingo aliiomba jamii ya Mikocheni kuwa walezi wazuri na kufuatilia mwenendo mzima wa watoto wao ili tuweze kutokomeza masuala yote ya ukatili wa watoto wote ndani ya Kata hii na Wilaya nzima ya Kinondoni.

Katika uzinduzi huo Mheshimiwa Mandingo alitoa mitungi ya gesi 20 yenye uzito wa Kilogramu 14.8 kwa Wanawake wajasiriamali wa Kata ya Mikocheni kwa lengo la kuokoa matumizi ya kuni.







# JIJI LA DODOMA LAIPONGEZA KINONDONI KWA UWEKEZAJI

Na
KAUNGA MAULID

Halmashauri ya Manispaa ya Jiji la Dodoma imeipongeza Manispaa ya Kinondoni kwa uwekezaji wenye tija na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo yenye ubora.

Pongezi hizo zilitolewa Aprili 16, 2024 na Mstahiki Meya wa Jiji hilo, Mheshimiwa Prof. Davis Mwamfupe, aliyewaongoza Madiwani na Wataalam katika ziara ya mafunzo ya siku moja ndani ya Manispaa ya Kinondoni. Ujumbe wa Madiwani hao ulitembelea Kituo cha Mabasi Mwenge na Ujenzi wa uwanja wa Mpira kilichopo Mwenge.

Mstahiki Meya Profesa Mwanfupe alisema, "Binafsi naipongeza Manispaa ya Kinondoni kwa uwekezaji mkubwa hasa katika mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi cha Mwenge sambamba na ujenzi wa uwanja wa mpira. Miradi hii itakuza na kuinua kwa haraka ukusanyaji wa mapato ya Manispaa, hivyo na sisi tunapaswa kuyaiga haya ili kuharakisha maendeleo ya Jiji letu,"



Kwa upande wake Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Mheshimiwa Songoro Mnyonge, alisema, licha kupongeza ujio huo pia alishauri kuwepo na uwekezaji ndani ya Jiji la Dodoma ili kurahisisha ukuaji na ongezeko la ukusanyaji wa mapato.

Nae Afisa Biashara wa Manispaa ya Kinondoni, Bw. Philipo Mwakibete, alishauri Mamlaka hizo mbili kuchangamkia fursa za uwepo wa fainali za kombe la Afika (AFCON) kwa kufanya uwekezaji mkubwa ambao utachangia kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa mapato”.

# CHUKUENI TAHADHARI DHIDI YA MVUA - M.D KINONDONI







Na
**KAUNGA MAULID**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Bi. Hanifa Suleiman Hamza, amewataka wakazi wa Kinondoni waliopo kwenye maeneo hatarishi kuchukua tahadhari dhidi ya mvua zinazoendelea kunyesha.

Rai hiyo aliitoa leo April 26, 2024 wakati alipotembelea maeneo yote yaliyokumbwa na maji sambamba na kutoa pole kwa wahanga wa maeneo hayo.

**"Usipime Nguvu ya Maji"**

***Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Bi. Hanifa Suleiman Hamza, akipokea maelezo juu ya athari ya mvua kutoka kwa Mchumi na Mratibu wa Maafa kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bw. Bakar Mlanzi***

Alisema,"Poleni sana kwa majanga haya. Lakini nawaombe sana muendelee kuchukua tahadhari pindi mnapoona mvua imezidi ili kuepuka kutokea kwa madhara makubwa."

Kadhalika,Mkurugenzi Hanifa aliwataka Wenyeviti wa Mitaa kuendelea kuwapa elimu na kuwahamasisha Wananchi kuchukua tahadhari kwenye maeneo yao ikiwemo wazazi kuwa makini kwa watoto wao katika kipindi hiki.

# KINONDONI YATOA TAHADHARI KWA WAKULIMA

**Na SAUMA MWANSHULI**

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kupitia Divisheni ya Mipango na Takwimu imewataka Wakulima kuchukua tahadhari dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi kwa kujikita katika kilimo kinachoendana na mabadiliko hayo.

Hayo yamebainbishwa leo Aprili 23, 2024 na Mchumi na Mratibu wa Maafa Manispaa ya Kinondoni Bw. Bakar Mlanzi wakati akiwa katika mafunzo kwa Wakulima ya namna ya kukabiliana na maafa ambayo yanasababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi.

“Kwasasa kumekuwa na mbadiliko makubwa sana hivyo ni muhimu sana kwa wakulima kutumia mafunzo haya kwa kutumia mafunzo haya kukabiliana na athari hizi za mabadiliko ya tabia ya nchi hasa kipinmdi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha, hivyo amewataka wakulima hao kukabiliana na madilliko ya tabia nchi kwa kuanzisha vikundi vitakavyowawezesha kuanzisha kilimo kitachohimili mabadiliko ya tabia ya nchi sambamba na kushiriki katika mafunzo mbalimbali ya kilimo ili kuleta teja katika kilimo," alisema Bw. Bakari.

Aidha Bw. Bakari alisema kuwa kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na mvua zinazoendelea kunyesha wakulima wanatakiwa kukabiliana na madilliko hayo kwa kuhifadhi mazao kutokana mvua kuwa nyingi ambayo imapelekea kuharibu mazao shambani na kusababisha upungufu wa chakula.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Divisheni ya Kilmo, Mifugo na Uvuviyalitolewa katika Kituo cha Mafunzo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Malolo kilichopo Mabwepande, Manispaa ya Kinondoni.



*Mchumi na Mratibu wa Maafa kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bw. Bakar Mlanzi akitoa wakati mafunzo kwa Wakulima kutoka Manispaa ya Kinononondoni juu ya namna ya kukabiliana na maafa ambayo yanasababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi katika Kituo cha kutolea mafunzo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Malolo kilichopo Mabwepande. (***Picha na Sauma Mwanshuli***)*

# MIAKA 60 YA MUUNGANO IONDOE VIKWAZO VYA BIASHARA

**Na**
**MWANDISHI WETU**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila ameitaka miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar iwe ni chachu ya kuondoa vikwazo vya biashara na kukuza mitaji kwa Wafanyabiashara wadogo.

Ametoa kauli hiyo leo April 22, 2024 alipoongoza Dua na Sala ya kuliombea Taifa ikiwa ni sherehe na wiki ya kuzindua Maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano iliyofanyika Manispaa ya Kinondoni.

Mhe. Chalamila amesema, "Wafanyabiashara wapewe Uhuru wa kufanya shughuli zao kwa masaa 24 ili kupata muda wa kutosha kujiongezea kipato na kukidhi mahitaji yao sambamba na kuongeza mapato ya nchi".

Ameongeza kuwa baadhi ya viongozi waache kuweka vikwazo kwenye baadhi ya biashara sambamba na kuzuia utoaji na upokeaji wa rushwa.

Mhe. Chalamila amesisitiza kuwa, maendeleo yaliyofanyika katika miaka 60 ya Muungano yawe ni chachu ya mafanikio. "Uwepo wa mwendokasi iwe ni chachu ya kukuza biashara zetu kwa kufika haraka maeneo ya biashara".

Aidha, Mhe. Chalamila amewataka wana Kinondoni kuona jinsi serikali ilivyopanua uwanja wa elimu, uwekezaji na Uhusiano wa Kimataifa kama chachu ya kukua kiuchumi kwa kutumia fursa zilizopo kwa kuacha kulalamika, kudumisha umoja na kuendelea kufurahia matunda ya Muungano huo.

Amesema, "kila mmoja atazame cheo Cha Rais kama mshumaa ambao ni lazima aungue ili wengine wapate mwanga", hivyo ni jukumu la kila mmoja kuhangaika uwepo wa umoja, mshikamano na upendo sambamba na kuondokana na mgawanyo ili kuendeleza Mungano ambao viongozi wetu waliuhangaikia kwa muda mrefu.

Mhe. Chalamila ameongeza kuwa, kupitia



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Albert Chalamila akiwa katika aongoza zoezi la kuliombea taifa yaliyofanyika katika ukumbi wa soko kuu la Magomeni Manispaa ya Kinondoni.*

*Kutoka Ukurasa......*

mshikamano wa viongozi imepelekea kukua kwa masalahi ya Uchumi, Siasa na Diplomasia.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Mkoa wa Dar es salaam (JMAT) Shekhe Mohamed Mawinda amesema kuwa kuelekea miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Vijana waelimishwe kuhusu umhimu na faida za Muungano.

Aidha, Shekhe Mawinda, amesema kuwa asilimia kubwa ya Vijana wameukuta Muungano hivyo wapewe Elimu ya umhimu na faida zake ili nao waweze kuulinda kutokana na umhimu wake kwa Taifa letu.

Kadhalika, Shekhe Mawinda amesema kuwa siku ya leo ni kipekee sana kwa Nchi yetu kwani kupata wasaa wa kumshukuru Mungu na kuliombea Taifa ni fursa ya kipekee sana katika ulinzi wa kile alichotujalia hususani amani na upendo.

"Watu wengi sana wamepoteza kila walichojaaliwa na Mwenyezi Mungu kwa kusahau kutoa shukrani kwa Mungu" ameongeza Shekhe Mawinda.

# MAFANIKIO YA MIAKA 60 YA MUUNGANO MANISPAA YA KINONDONI

**Na JAMILA MDEMU**

Tunapoadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuendelea kuimarisha umoja, amani, na utulivu ambavyo vimepelekea kukua katika Sekta ya Uchumi, Elimu, Uwekezaji, Afya, Kilimo, Biashara na Maendeleo ya jamii.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa April 26, 1964 ikiwa ni Muungano wa Mataifa mawili huru ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya watu wa Zanzibar ambayo yaliingia mkataba ya Muungano mnamo mwaka 1964 na kuanzisha Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekuwa na ushirikiano mzuri na Zanzibar ambapo kumekuwa na ugeni kutoka Manispaa zilizopo Zanzibar kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika masuala mbalimbali yatakayowezesha utendaji kazi kwenye Halmashauri zao ambapo ziara hizo zimekuwa zikijumuisha Madiwani na Watendaji kutoka Zanzibar kwa kutembelea miradi mbali mbali inayoendelea kutekelezwa katika Manispaa ya Kinondoni

Vile vile Wageni kutoka Manispaa ya Magharibi B walifanya ziara katika Manispaa ya Kinondoni kwa lengo la kujifunza usimamiaji uwekezaji katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo walitembela fukwe za Coco, Kiwanda cha kuchakata mbolea ya mboji kilichopo Mabwepande, Uwanja wa mpira na kituo kipya cha Bus kilichopo Mwenge.

Katika kuelekea kuadhimisha Miaka 60 ya Muungano, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni iliandaa Dua na Sala kwa ajili ya kuliombea Taifa mnamo tarehe 22 April, 2024 ambapo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert John Chalamila alihudhuria na kuitaka miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar iwe ni chachu ya kuondoa vikwazo vya biashara na kukuza mitaji kwa Wafanyabiashara wadogo.

***BIASHARA MASAA 24 KINONDONI***

Mhe. Chalamila alisema, "Wafanyabiashara wapewe Uhuru wa kufanya shughuli zao kwa masaa 24 ili kupata muda wa kutosha kujiongezea kipato na kukidhi mahitaji yao sambamba na kuongeza mapato ya nchi". Aliongeza kuwa baadhi ya viongozi waache kuweka vikwazo kwenye baadhi ya biashara sambamba na kuzuia utoaji na upokeaji wa rushwa.

Mhe. Chalamila alisisitiza kuwa, maendeleo yaliyofanyika katika miaka 60 ya Muungano ikiwemo uboreshaji wa miundombinu iwe ni chachu ya mafanikio. "Uwepo wa mwendokasi iwe ni chachu ya kukuza biashara zetu kwa kufika haraka maeneo ya biashara".

Aidha, Mhe. Chalamila aliwataka wana Kinondoni kuona jinsi serikali ilivyopanua uwanja wa elimu, uwekezaji na Uhusiano wa Kimataifa kama chachu ya kukua kiuchumi kwa kutumia fursa zilizopo kwa kuacha kulalamika, kudumisha umoja na kuendelea kufurahia matunda ya Muungano huo.

Aidha, aliongeza kuwa Miaka 60 ya uhuru imekuwa ni chachu ya kupanua uwanja wa elimu, uwekezaji na uhusiano

*Kutoka Ukurasa......*

wa Mataifa makubwa ambayo yamekuwa ni fursa ya maendeleo kwa Watanzania ikiwemo kuweza kufanya biashara na maeneo mbalimbali na kukuza mapato ya nchi.

Mhe. Chalamila alisisitiza kuwa, kupitia mshikamano wa viongozi kwa kutokuwa na uchoyo pamoja na uroho wa madaraka imepelekea kukua kwa maslahi ya Uchumi, Siasa na Diplomasia.

Nae, Afisa Biashara, Bw. Philipo Mwakibete alizungumzia kauli ya wafanyabisahara kutowekewa vikwazo kwa kusema, " wafanyabiashara wana wajibu wa kuzingatia na kufata sheria zilizowekwa na mamlaka husika kwani uvunjifu wa taratibu hupelekea uvunjifu wa sheria ". Ameongeza kuwa ili wafanyabiashara wasiwekewe vikwazo ni lazima wafate sheria zilizowekwa.

Bw. Mwakibetw amesisitiza kuwa, uanzishwaji wa kufanya biashara kwa masaa 24 itaongeza mapato kwa Manspaa ya Kinondoni lakini ni suala la kuendea taratibu katika eneo dogo ili kujipanga kwa eneo kubwa hata kufikia nchi nzima ". Katika kulifikia hili kujipanga ni muhimu ikiwemo kuandaa sheria za usalama, sheria za biashara, sheria za mipaka pamoja na sheria za uhamiaji".

***USAWA WA KIJINSI KATIKA UONGOZI***

Nae, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza alisema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umesaidia Kinondoni kusonga mbele katika kila Sekta kutokana na kuwepo kwa Umoja na Mshikamano vinavyopelekea uwazi, ushirikishwaji na kujadili mambo ya maendeleo.

Aliongeza kuwa, Muungano umesaidia kuwepo kwa usawa katika Uongozi ambapo wanawake wameweza kupata fursa ya kuwa viongozi katika ngazi tofauti akitoa mfano wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan ambaye anaongoza nchi.

Vile vile, Bi. Hanifa alisisitiza kuwa Muungano umesaidia kukua Sekta ya Viwanda, kutanuka kwa biashara, kuwepo kwa masoko ambayo yamesaidia wananchi kujiajiri na kusaidia kila Sekta kukua na kuleta maendeleo katika Manispaa. "ndani ya miaka 60 ya Muungano Maniapaa ya Kinondoni imefanikiwa kuwa na shule za msingi na sekondari katika Kata zote sambamba na kuwepo kwa huduma za afya katika Kata zote".

***ULINZI WA MUUNGANO***

Mhe. Chalamila aliwataka Watanzania kuulinda Muungano kwa kutowagawa watu kutokana na tabia za baadhi ya watu kuwa na makundi. "Tanzania ni moja ya nchi chache Duniani zenye mfano wa Muungano kudumu hivyo kila mmoja atazame cheo Cha Rais kama mshumaa ambao ni lazima aungue ili wengine wapate mwanga hivyo ni jukumu la kila mmoja kuhangaikia uwepo wa umoja, mshikamano na upendo sambamba na kuondokana na mgawanyiko ili kuendeleza Muungano ambao viongozi wetu waliuhangaikia kwa muda mrefu.

Naibu Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe, Joseph Rwegasira ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Makongo aliongeza kuwa, kila mmoja ana sababu ya kuulinda, kusimamia na kuupigania Muungano. "Maendeleo tuliyo nayo yanatokana na Muungano uliopo hivyo hatuna budi kuupigania na kuutetea kwani umeondoa ubaguzi, kuna muingiliano baina ya Bara na Visiwani sambamba na kuwepo kwa uhuru wa kuabudu". Amesema, Mhe. Rwegasira.

"Waasisi wa nchi yetu walipambania Muungano hivyo tusiuharibu. Tuendelee kuulinda ili kuendelea kuilinda amani iliyopo". Aliongeza Mhe. Rwegasira.

Viongozi wa dini pia walisisitiza kuulinda Muungano uliopo kwani umeleta manufaa makubwa kwa Taifa letu ikiwemo kuwaunganisha wafanyabiashara na kuwepo na muingiliano baina ya Visiwani na Bara pasipokuwa na kikwazo chochote.





# MIRADI MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Jengo la Utawala la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni*



*Muonekano wa Kituo cha cha kisasa cha Mabasi kilichopo Mwenge*



*Muonekano wa Nyumba ya Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mbweni Tetailiyopo Kata ya Mbweni Manispaa ya Kinondoni.*



*Muonekano wa Uwanja wa mpira wa timu ya KMC FC uliopo Mwenge*



***Muonekano wa Hospitali ya Wilaya ya Kinondoni ilipo Mabwepande***




*Mupnekano wa Soko Kuu la Magomeni lililopo Manispaa ya Kinondoni*





# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Saad Mtambule akiwa katika kongamano la Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.*



*Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule akikabidhi boksi 56 za vitakasa mikono kwa Maafisa elimu Msingi na Sekondari wa Manispaa ya Kinondoni.*



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe. Songoro Mnyonge akiwa na wageni kutoka Dodoma.*



*Meya wa Manispaa ya Kinondoni na Diwani wa Kata ya Mwananyamala Mhe. Songoro Mnyonge (katikati) akiserebuka sambamba na Diwani wa Viti Maalum Mhe. Rehema Mandingo (kushoto) katika uzinduzi wa usafi wa mazingira na matumizi ya nishati safi uliofanyika katika Kata ya Mikocheni.*



*Afisa Usimamizi wa Taka na Usafishaji wa Mazingira Bi. Nancy Zakayo akikabidhi Mche wa Mti ikiwa ni moja ya kampeni ya mguu kwa mguu kitaakatika zoezi la upandaji miti*



*Katibu Tawala wa Wilaya ya Kinondoni Bi. Stella Msofe akishuhudia zoezi la uchanjaji wa chajo ya HPV kwa watoto wadogo katika Shule ya Msingi ya Ali Hassan Mwinyi*




*Wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Ali Happi waadhimisha miaka 60 ya Muungano kwa kupanda miti.*



*Wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Ali Happi waadhimisha miaka 60 ya Muungano kwa kupanda miti.*



*Wananchi wakiwa katika kampeni ya usafi wa Mguu kwa Mguu Kitaa*

# UKURASA WA MAKALA ZETU



# MGUU KWA MGUU KITAA KUIFIKIA KINONDONI KWA ASILIMIA 100

## ●*Jumanne na Alhamis Zaongezwa kuwa siku Maalum za Usafi Kinondoni*
## ●*Ujenzi wa Karo Wahimizwa kwa Wananchi*



*Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Taka na Usafishaji wa Mazingira Manispaa ya Kinondoni, Bw. Shedrack Maximillian akiiongoza timu ya mazigira katika kampeni ya "Mguu kwa Mguu Kitaa" ili kusikiliza na kutatua changamoto za usafi wa mazingira kwenye Mitaa hiyo.*

**Na Kaunga Maulid, KMC Media**

Hivi karibuni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kupitia Kitengo cha Usimamizi wa Taka na Usafishaji wa Mazingira, imezindua kampeni ya usafi wa mazingira ya "Mguu kwa Mguu Kitaa" iliyolenga kutembelea, kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazohusu taka na usafi wa Mazingira kwenye Mitaa yote ya Manispaa ya Kinondoni. Kampeni hii imekuwa na matokeo chanya katika Mitaa mbalimbali. Matokeo hayo chanya yanajionesha kwa mafanikio ya kiwango cha asilimia 100. Hii inatokana na kampeni hiyo kupokelewa kwa mikono miwili ndani ya Kata zote kwa Wananchi kuwajibika kushiriki katika kufanya usafi kwenye maeneo yao, kuzibua mitaro ya maji machafu ambayo ni chechefu katika mitaa hiyo. Akiongea katika uzinduzi wa kampeni hiyo hivi karibuni katika Kata ya Makongo Mtaa wa Mlalakuwa, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Mheshimiwa Saad Mtambule, anasema usafi ni jukumu la kila mtu hivyo ni wajibu kwa Mwananchi kushiriki katika kufanya usafi kwenye maeneo yanayowazunguuka. Aidha Mheshimiwa Mtambule anasisitiza kuwa, suala la usafi ni moja ya vipaumbele ndani ya Manispaa ya Kinondoni, hivyo ni lazima kama mkazi wa Manispaa ya Kinondoni kuendelea kuweka ulinzi madhubuti katika maeneo yanayowazunguuka. Anasema, "ili tuweze kupambana na magonjwa ya mlipuko kama Kipindupindu, lazima tuweke kipaumbele katika masuala mazima ya kufanya usafi na kupendezesha mazingira yetu kwa pamoja." Mheshimiwa Mtambule pia anahimiza suala la ulinzi dhidi ya wanaochafua mazingira kwa kuwataka kuwakamata watu wa aina hiyo ili wawajibishwe kwa mujibu wa Sheria za Mazingira. Manispaa ya Kinondoni imekuwa na utaratibu wa kufanya usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa usafi, Mkuu wa Wilaya anaongeza kuwa, "Manispaa ya Kinondoni imejidhatiti katika hilo kwa kuweka siku mbili za kufanya usafi wa pamoja ndani ya wiki ambayo ni Jumanne na Alhamisi." Anasema hatua hii ni kuchagiza kasi ya kufanya usafi kwenye maeneo mbalimbali ya Mitaa yote ya Manispaa ya Kinondoni. Kwa upande wak,e Naibu Meya wa Manispaa ya Kinondoni ambae pia ni Diwani wa Kata ya Makongo, Mheshimiwa Joseph Rwegasira, ameipongeza kampeni ya "Mguu Kwa Mguu Kitaa." Anasema kuwa ubunifu huo utaleta manufaa makubwa katika

*Kutoka Ukurasa......*

kupunguza changamoto za taka kwenye Mitaa mbalimbali. Anasema, "Naipongeza Manispaa ya Kinondoni kwa kuanzisha kampeni hii. Kupitia kampeni hii, maeneo mengi yenye changamoto za taka yatapatiwa suluhu," na kuongeza kuwa, "hakikisheni kampeni hiyo inafika katika Mitaa yote 106." Ulipaji wa fedha za ada ya taka ni moja ya ajenda kubwa ilikuwa ikisisitizwa katika kampeni hiyo ili kurahisisha ukusanyaji wa taka hizo ndani ya Mitaa na kuweka mazingira safi na salama. Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Taka na Usafishaji wa Mazingira Manispaa ya Kinondoni, Bw. Shedrack Maximillian, amesema, "kila Kaya ina wajibu wa kushiriki katika suala zima la usafishaji wa maeneo yanayowazunguka na ulipaji wa ada ya taka kwa wakati ambalo ni jambo la kisheria." Aidha, Bw, Shedrack, amewataka Wakandarasi wanaohusika na ukusanyaji wa taka katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Kinondoni kuhakikisha wanakusanya taka hizo ili zisikae kwa muda mrefu. Amewasisitiza Wakandarasi hao kuweka utaratibu wa kupeleka





**Picha Mbalimbali zikionesha maeneo ya Mitaa ambayo kampeni ya Mguu kwa Mguu imeifikia**

gari la taka mara mbili kwa wiki kwenye mitaa hiyo ili kukusanya taka kwa urahisi kwenye maeneo yote. Mbali na utolewaji wa elimu, kusikiliza na kutatua kero za usafi wa mazingira, Kitengo hiki pia kimeweza kuongoza zoezi la upandaji miti katika Mitaa mbalimbali. Afisa Usimamizi wa Taka na Usafishaji wa Mazingira Bi. Nancy Zakayo, anasema, "mazingira ni miti na miti ni mazingira, pandeni miti, muitunze na kupendezesha mazingira ili kuendana na kampeni ya kuiweka Kinondoni ya Kijani." Wanasema "Mnyonge mnyongeni ila Haki yake Mpeni" Kongole na Pongezi nyingi ziende kwa Manispaa ya Kinondoni kupitia Kitengo cha kwa Usimamizi wa Taka na Usafishaji wa Mazingira kwa uzinduzi na usimamizi wa kampeni hii. Baadhi ya Wananchi wameipongeza Manispaa ya Kinondoni huku wakioneshwa kuipokea kampeni hiyo kwa mikono miwili. "Tunaishukuru kwa kuanzisha kampeni hii ambayo itatusaidia kuweka mazingira yetu safi na salama," Anaeleza Bw. Godfrey Mussa na kuongeza kuwa, "Wakandarasi wa taka wahakikishe wanafanya kazi yao kwa wakati ili kuepusha mlundikano wa takataka kwenye Mitaa yetu. Usafi ni jukumu letu sote kila mmoja awajibike kwa nafasi yake ili tutunze mazingira kwa pamoja.



# "LISHE SIO KUJAZA TUMBO, ZINGATIA UNACHOKULA"

**Na DIANA KAMASHO**

Lishe Sio Kujaza Tumbo, Zingatia Unachokula" hii ni moja ya kauli mbiu ya mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 iliyohamasisha ulaji wa vyakula bora na unaofaa.

Katika kuelekea mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2024, suala la lishe ni moja ya masuala mtambuka ambayo yamekuwa yakipewa kipaumbele na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Lengo ni kuhakikisha afya bora kwa watoto sambamba na watu wote ndani ya Manispaa ya Kinondoni.

Ikiwa Manispaa ya Kinondoni inajiandaa kupokea mwenge wa Uhuru 2024, imeendelea kutoa mafunzo ya lishe ya Mtaa kwa Mtaa na Shuleni ikiwa ni moja ya kuunga mkono ujumbe wa mbio za Mwenge isemayo "Lishe sio Kujaza Tumbo, Zingatia Unachokula".

Moja ya mikakati ambayo imewekwa na Manispaa ya Kinondoni kupitia Divisheni ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Divisheni ya Mifugo, Kilimo na Uvuvi ili kuimarisha lishe ndani ya jamii, imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutoa elimu juu ya lishe kwa Mtaa kwa Mtaa, kuunda klabu za kwa watoto Shuleni na jamii kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Afisa Lishe, Bi.Emiliana Sumaye, hadi sasa, ikiwa ni siku chache kuelekea mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Manispaa ya Kinondoni imefanikiwa kutoa elimu katika Mitaa yote 106 ya Kata 20.

Mafunzo haya yamekuwa yakitolewa mara kwa mra ikiwa na lengo la kuhamasisha jamii ulaji wa vyakula vyenye lishe.

Akiongea katika mafunzo hayo Katanya Mikocheni, Afisa Lishe Bi. Sumaye anasema mafunzo hayo yamekuwa na manufaa makubwa kwani jamii imekuwa na mwamko mkubwa katika uandaaji wa chakula chenye lishe.

Anasema, "Kwa mwaka huu 2023/2024 hali ya lishe ndani ya Manispaa ya Kinondoni inakabiliwa na changamoto ya lishe duni ambapo kuna udumavu kwa asilimia 7.8, ukondefu na upungufu wa uzito kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano."

Sambamba na hayo Bi. Sumaye amesema kuwa, bado kuna changamoto ya upungufu wa damu kwa watoto sambamba



*Afisa Lishe kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bi. Emmiliana Msangi akitoa mafunzo juu ya namna ya uandaaji wa lishe bora kwa watoto na watu wazima.*



***Kutoka Ukurasa......***

na Wajawazito ambao unasababishwa na ukosefu wa lishe bora.
Amesema kuwa kutokana na changamoto hizo, "Manispaa ya Kinondoni imeweka mikakati madhubuti katika kuhakikisha inakomesha suala hilo ikiwepo semina, mikutano ya hadhara, majukwaa mbalimbali, maadhimisho ya kitaifa, kimkoa na wilaya na mafunzo shuleni juu ya Lishe."
Kwa upande mwingine, Manispaa imekuwa ikifanya kazi sambamba na Afya Check na Outreach (Clinic Mkoba) na wataalam katika maeneo yao ili kuhakikisha jamii inapata elimu ya lishe ambayo imekuwa ni changamoto kubwa kwao.
Bi. Sumaye ameongeza kuwa kumekuwa maadhimisho ya siku za lishe katika mitaa mbalimbali katika kila robo mwaka kwa kila mtaa ambapo wamekuwa wakitoa elimu ya lishe kwa vitendo kwa wananchi.
Aidha, Wataalamu wa afya na watoa huduma ngazi ya jamii, wamejengewa uwezo ili waweze kuelimisha jamii kuhusu lishe bora wanapowatembelea katika vituo vya afya au wakati wa ziara za nyumba kwa nyumba.
Jamii inahamishwa kilimo cha mazao hasa kilimo mjini kama matunda, mboga mboga, na mazao mengine. Pia ufugaji wa wanyama wadogo wadogo kama Sungura, na Kuku wanaoweza kusaidia katika upatikanaji wa chakula mchanganyiko kwa bei nafuu.
Msisitizo mwingine katika Lishe umekuwa ni Kusimamia ubora wa chakula kinachouzwa katika masoko ili kuhakikisha kuwa ni salama na kinachofaa kwa matumizi ya binadamu.
Baadhinya changamoto zinazoikumba jamii katika masuala ya Lishe ni pamoja na ukosefu wa elimu kuhusu liishe bora, udhibiti ubora wa chakula, na uangalizi mdogo kwa watoto wadogo huchangia kudhoofu hali za lishe za watoto wadogo. Changamoto hizi zimekuwa nimfursa kwa Manispaa kuhakikisha inapambana nazo katika ngazi ya familia na Mitaa.
Karibu Mwenge wa Uhuru 2024 Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.



*Akina Mama mbalimbali kutoka Kata ya Bunju wakiwa katika mafunzo ya namna ya uandaaji wa chakula chenye lishe bora yiliyotolewa kwna Wataalam wa lishe kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.*

# KINONDONI YAPUNGUZA MAAMBUKIZI YA MALARIA

- ***15,600,000.00 zanunua Lita 1,181 za viatilifu kuua viluwiluwi***
- ***Vyandarua vyenye thamani ya 719,430,000.00 vyagawiwa***
- ***63,454,471.49 zatengwa kudhibiti***

**Na**
**ELINA PASCAL (UoI)**



Wakati takwimu za kitaifa zikionesha kupungua kwa maambukizi ya ugonjwa wa Malaria kwa asilimia 45 kutoka asilimia 14.8 ya mwaka 2015 hadi asilimia 8.1 ya mwaka 2022, Manispaa ya Kinondoni kwa upande wake imeendelea na juhudi za kupambana na ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Divisheni ya Afya, hali ya maambukizi kinaonesha kupungua kutoka asilimia 1.5 kwa kipindi Cha Julai 2022 hadi Machi 2023 hadi asilimia 0.42 kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Hii ni sawa na wagonjwa wa Malaria walikuwa 20,340 sawa na ya wagonjwa wote 2,782,102 waliotibiwa katika vituo vya kutolea huduma ya Afya ndani ya Wilaya ya Kinondoni.

Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya Divisheni hiyo, pia pamekuwepo na kupungua kwa vifo vitokanavyo na Malaria kutoka vifo 14 kwa kipindi Cha Julai 2022 hadi Machi 2024.

Manispaa imeweza kukabiliana na maambukizi haya kwa kuchukua hatua mbalimbali za kinga na tiba. Moja ya hatua hizo ni ugawaji wa vyandarua 47,962 bila malipo kwa wajawazito na watoto katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024.

Aidha, Wajawazito 27,134 sawa na asilimia 91 waliokwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya, walipewa vyandarua, wakati vyandarua 20,828 viligawiwa kwa watoto waliokwenda kliniki kwa chanjo ya Surua ya miezi 9 sawa na asilimia 72 ya watoto waliochanjwa.

Naye Mratibu wa Afya ya Mzazi na Mtoto Bi. Fausta Kambanga, anaelezea kuwa njia nyingine ya kudhibiti ugonjwa huu ni pamoja na kutoa elimu ya afya ya kujikinga na Malaria kwa wajawazito wanaokuja Kliniki. Aidha kwa kutumia kipimo cha MRDT, wagonjwa wanaogundulika kuwa na maambukizi ya Malaria hutibiwa haraka, ikiwemo matibabu bure kwa mtoto asiyezidi umri wa miaka Mitano.

Manispaa ya Kinondoni pia inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kupambana na Malaria. Wadau hao ni pamoja na Taasisi ya Afya ya Ifakara (IHI), Family Health Institute (FHI), JHPIEGO, vyombo vya habari na wanajamii wa kujitolea.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Bi Hanifa Suleiman Hamza, mara kwa mara amekuwa akisisitiza umuhimu wa kufanya usafi katika maeneo ya makazi ili kuepusha madhara ya kiafaya yakiwemo maambukizi ya Malaria.

Katika kusherehekea mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2024, yenye kauli mbiu ya Ziro Malaria Inaanza na Mimi; nachukua hatua kuitokomeza, Manispaa inajitanabaisha kwa kufanikiwa kupunguza maambukizi haya.

**Na**
**DIANA KAMASHO**



Kituo cha afya cha Kinondoni ni moja ya mradi mkubwa uliotelekezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ukiwa na matokeo makubwa sana katika Kata ya Kinondoni. Kwa takribani miaka 62 sasa wakazi wa eneo hili waliishi bila ya kuwa na kituo cha afya jambo ambalo liliwalazimu kufata huduma katika hospitali za jirani kama Mwananyamala au Muhimbili.

Katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi hiyo Mbunge wa jimbo la Kinondoni Mhe Abassi Tarimba ameishukuru sana serikali kwa kuwakumbuka wakazi wa eneo la Kinondoni kwani ilikua ni kilio chao kikubwa.

“Ninashukuru sana serekali ya Dkt Samia Suluhu kwa kutukumbuka wana Kinondoni kwani tumeishi miaka 60 ya uhuru bila uwepo wa kituo cha afya" alieza.

Kituo hichi cha Kinondoni nimiongoni mwa vituo bora vya afya kikiwa na gharama ya takribani shilingi 1,641,561,979.60 chenye ukubwa wa gorofa moja lenye wodi ya mama na mtoto, sehemu ya upasuaji pamoja na wodi ya ndani IPD.

Katika maboresho hayo ya huduma za Afya katika manispaa ya Kinondoni wamefanikiwa pia kupunguza kero ya ukosefu wa magari ya wagonjwa wa dharura(ambulence) jambo ambalo limepelekea kupunguza vifo kwa wakazi wa maeneo mbalimbali.

"katika maboresho tuliyofanikiwa ni pamoja na kuongeza ambulance za wagonjwa katika baadhi ya vituo vya Afya kama Mabwepande na Kigogo"alieleza Dr Ngereza Kaimu mganga Mkuu Manispaa ya Kinondoni.

Mbali na hayo Ofisi ya Mkanga Mkuu wa Manispaa ya Kinondoni imeweza kuhuhakikisha inafanya ufatiliaji wa Huduma za Afya katika vituo vyote vya Manispaa kwa kutembelea kila siku, kutoa namba za simu pale inapotokea changamoto yoyote ya kutolewa hii yote ni kuakikisha ufanisi katika vituo vya afya vya Kinondoni Lakini pia kuna timu ya wawakilishi wanachi.

"Tunatoka kila siku kufatilia vituo ngazi zote lakini namba tumetoa hivyo tunapokea simu nyingi sana"alieze Dr Ngeleza.

Kufuatia ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Albert Chalamila Manispaa ya Kinondoni iliyojikita katika uimarishaji wa vituo vya afya kwa kuvifanya viwe na uwezo wa kutoa huduma za dharura na zisizo za dharura kwa ufanisi.

Mhe Albert Chalamila ameipongeza sana Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa jitihada na ufanisi wanaouonyesha katika kuhakikisha wanayatimiza maono ya Serekali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya utoaji wa huduma bora za afya.

Ambapo kituo cha Kinondoni kitaweza kusaidia takribani wakazi 85358 katika Kata ya Kinondoni, Mwananyamala na maeneo mengine jirani ya Wilaya ya Ilala.



*Muonekano wa jengo la Kituo kipya cha Afya cha Kinondoni*

# TIMU YA WATUMISHI MANISPAA YA KINONDONI YAJIWEKA MGUU SAWA

**Na**
**ATHUMAN NTAFUMILA**

Timu ya Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, imecheza na timu ya Waandishi wa Habari za michezo (TASWA) katika Viwanja vya Bora vilivyopo Kata ya Kijitonyama.

Mechi hiyo ya kirafiki ilihusisha michezo miwili kwa maana ya mpira wa Pete kwa upande wa Wanawake na mpira miguu kwa Wanaume, lengo kuu likiwa ni kuongeza utimamu wa miili na akili kwa Watumishi hao.

Akiongea, mara baada ya michezo hiyo Mwenyekiti wa Timu ya Watumishi Bi. Juliana Mboma amesema kuwa, mechi hiyo imefanyika Ili kutekeleza agizo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Hamza ambaye amewataka wote kushiriki katika michezo mbalimbali kwa Afya ya mwili na akili Ili kuongeza ufanisi wa kazi na kutoa bora kwa Wananchi.

"Tunajitahidi kutafuta michezo ya kirafiki Ili kuhakikisha tunajiweka sawa kimwili na kiakili Ili tuwahudumie.









# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI



**Mhe. SAAD MTAMBULE**
**Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni**

**Bi. STELLA MSOFE**
**Katibu Tawala wa Wilaya ya Kinondoni**

**Mhe. SONGORO MNYONGE**
**Meya Manispaa ya Kinondoni**

**Bi. HANIFA SULEIMAN HAMZA**
**Mkurugenzi Manispaa ya Kinondoni**

***Jarida la Manispaa Ya Kinondoni 2023/2024***
***www.kinondonimc.go.tz***